
FEBRUARI MMXXIV - TOLEO LA XXIX

# NGURUMO
*ya mwandishi*



Ally Hassan
Mwinyi
1925 - 2024

# SIKITIKO

## YALIYOMO

**TAHARIRI**— SIKITIKO —Uk 02

**MWANDISHI WETU**— BENEDICHTER LIBERATUS — Uk 03

**New In Town:** BAYO NA IMBORI **—** uk 04

**PITIO LA VITABU**—
(Ikisiri) 8—Uk 06

**MAKALA— SAIKOLOJIA**: Usijitotoshe (marudio) —Uk 06 na 07

**RIWAYA:** Nilimuua Dada Niolewe Na Shemeji '14'— uk 08 na 09

**MIAMBA WA AFRIKA:** Muammar Gaddafi '04'— Uk 10

**Sako kwa Bako– Eva Mrema:** MWANAMKE MWENYE THAMANI NDANI YANGU **—**Uk 11

**RIWAYA:** — Unaye Rafiki? —Uk 12 na 13

**RIWAYA—** Cronoc 7 '11'- Uk 14 na 15

**YA KALE NI DHAHABU**: — Alibaba na Wezi 40 '8'- Uk 16

**HABARI:** Kwaheri Mzee A.H. Mwinyi – Uk 17

**SHUBAKA LA VITABU:** Zijue maktaba 10 bora duniani '5'—Uk 18

**KITABU NILICHOSOMA:** — SHOW YOUR WORK—Uk 19

**MATANGAZO: -** Uk20

**MALENGA WA KILEO —** Uk 21

**HABARI PICHA: -** Uk 22

**KUTOKA MAKTABA:** Miaka 62 ya Uhuru : Vituko Vya Uhuru**- '4'-**Uk 23

**ELIMU JAMII:** — Sheria ya ndoa katika mgawanyo wa mali—Uk 24 na 25

**NGURUMO YA MWANDISHI**

**WASILIANA NASI**
**0766 974 865 AU 0627160016**
**WhatsApp: +255 766974865**

## TAHARIRI: SIKITIKO

Wasalaam ndugu zangu!

Februari umemalizika  na Machi umeshafika, maisha yanaendelea kama ambavyo Mwenyezi Mungu amepanga. Twapaswa kumshukuru Mungu kwa yote ambayo ametujalia, si kwamba sisi tu wema sana au tu zaidi ya Yule mwingine, la. Bali upendo wake kwetu u mkubwa daima na usio na mipaka.

Yeye huwanyeshea mvua waove na wema, huwapa jua waovu na wema. Je ni upendo wa namna gani huu?

Nichelee kusema kwamba Februari wengi tumesherehekea siku za kuzaliwa kwetu, lakini wapo walioondokewa na wapendwa wao.

Sisi kama taifa la Tanzania, Februari hii imeondoka na wapendwa wetu wawili; aliyekuwa Waziri Mkuu katika awamu ya nne ya utawala, Mh. Edward Ngoyai Lowassa , alitwaliwa kwa Muumba wake.

Na katika tarehe ya mwisho kabisa ya Februari, Mzee wetu Ally Hassan Mwinyi, naye alitwaliwa. Wote hawa wawili tutawakumbuka kwa mema waliyotenda nje na ndani ya uongozi wao. Tutamkumbuka Edward Lowasa kwa upambanaji wake na maamuzi yenye tija kwa Watanzania. Aliamua na aliweza na matunda tumeyaona.

Tutamkumbuka Mzee Mwinyi, aliyewahi kuwa Rais wa Zanziba na Muungano, zaidi ya yote mlumbi na mwalimu mshititi wa lugha adhimu ya Kiswahili. Kwetu alikuwa baba na mpaka mwisho alikuwa babu, kwani ameondoka akiwa na miaka tisini na kenda. Almabusura afikishe 'karne'.

Mzee Mwinyi ametuachia mengi ya kujifunza.  Alikuwa rais wakati mgumu wa mageuzi ya kiuchumi na kisiasa. Kwa hekima aliyojaaliwa na Mungu aliweza kutuvusha salama kipindi hiko. Mwenyezi Mungu amjaalie pepo iliyo njema.

"(…) Maisha ya mwanadamu ni hadithi tu hapa ulimwenguni, basi ee ndugu yangu, kuwa hadithi nzuri kwa hao watakaosimuliwa. Hilo nnaloliomba (…)" - Ally Hassan Mwinyi

Mwenyezi Mungu azipokee roho za marehemu wapendwa wetu.

Mungu ibariki Afrika, Mungu ibariki Tanzania.

Richard Mwambe
29.2.2024
IRINGA

# MWANDISHI WETU: BENEDICHTER LIBERATUS

Naitwa Benedicther Liberatus na umri wa miaka 21, ni mwanachuo pia ni mwandishi wa simulizi, riwaya, tamthilia pamoja na miongozo ya film.

Kazi yangu ya uandishi nimeanza kipindi cha nyuma kidogo. Nilifanikiwa kutoa kitabu changu cha kwanza mwaka 2018 ambapo nilikuwa kidato cha tatu.

Mpaka sasa nimefanikiwa kutoa vitabu vitatu ambavyo vimekuwa vikifanya vizuri kwenye jamii kama vile kufundisha, kujenga, kuhamasisha, kuburudisha na kukosoa jamii.
Kitabu changu cha kwanza kinaitwa HII NI DUNIA YA NAMNA GANI? Na cha pili kinaitwa MACHOZI YA DHAHABU na cha tatu kinafahamika kama GUANTANAMO (SEHEMU YA MATESO).

Katika kila kitu huwezi kukosa changamoto, pia kwenye uandishi changamoto ni nyingi sana, licha ya kuwa mwandishi wa mda kidogo lakini bado changamoto zimekuwa nyingi nyingi kidogo, mfano watu wengi sikuhizi wamekuwa wa bize sana kuangalia film badala ya kusoma kama hapo mwanzo. Naweza kusema idadi ya watu wanaosoma vitabu imepungua sana tofauti na mwanzo au miaka ya nyuma ambapo watu wengi walikuwa wakisoma magazeti, vitabu na kadharika.

Ukiacha changamoto za mitaji, vifaa lakini hiyo ndio changamoto kubwa zaidi kwasababu mtu unawekeza nguvu nyingi lakini matokeo yana kuwa sivyo na ulivyotaraji.
Mimi binafsi sijawahi kujutia kuwa mwandishi kwasababu ni kitu ninachokipenda, yaani nakifurahia. Naweza sema kuandika pia ni starehe yangu kama ilivyo kwa mwingine, labda pombe au chakula fulani pia kwangu uandishi ni starehe yangu na napenda kuandika.

Uandishi umeninufaisha sana umenipa jina na pia umenikutanisha na watu wengi ambao kama isingekuwa uandishi basi naamini nisingekutana nao. Hivyo basi itoshe kusema mimi najivunia kuwa mwandishi na siwezi kuacha kuandika na huo ndo msimamo wangu.

Wanaonitazama kama *role model* au wanapenda kuwa waandishi kama mimi, nipende kuwashauri wasikate tamaa, uandishi ni kazi na waweke jitihada na kupambana na pia wasimsahau Mungu wao kwasababu yeye ndie mtoa riziki.

Vitabu vyangu kwa sasa havipo madukani ila hivi karibuni vitakuwepo kwenye maduka yote ya vitabu vya riwaya ila kwasasa kama unahitaji nitembelee kwenye kurasa zangu za mitandao ya kijamii.
Facebook, Instagram: Beneliberaty22 na Watsap: 0622570171.



Penda kusoma vitabu

www.richardmwambe.com JAMVI la SIMULIZI

**Faida za kusoma vitabu:**

- Msisimko wa Akili
- Kupunguza Msongo wa Mawazo
- Kuongeza Ujuzi wa mambo mbalimbali
- Kuongeza Msamiati
- Huboresha Uwezo wa Kukumbuka
- Hukupa Uwezo Mkubwa wa kuchambua na kufikiri
- Huboresha Mtazamo na Umakini

Benedichter Liberatus ni mmoja kati ya waandishi wa kike wanaokuja kasi sana katika tasnia hii.

Inawezekana kuwa hujamjua au hujawahi kukutana na kazi zake. Basi kwako isiwe tatizo, Ngurumo ya Mwandishi imemsogeza kwako ili umjue.

Usisite kumtembelea katika kurasa zake za mitandao ya kijamii kama alivyoelekeza mwenyewe ili uweze kuonja ladha ya uandishi wake.

Ngurumo ya Mwandishi twamtakia kila la kheri katika safari yake.

## NEW IN TOWN :
## BAYO NA IMBORI

***FASIHI kamwe haisimami na hakuna wa kuizuia kwani kila uchao mikono ya wanafasihi uweka maneno yenye ladha tamu vitabuni. Yote haya ili ujifunze, uburudike na kujirekebisha.***

***Katika tarehe hii ya mwisho kabisa ya Mwezi wa Februari Boniphae Daud Ngumije anatuletea kazi maridhawa kwetu walumbi wa Kisawahili. Bayo na Imbori kunani?***

***Hii ni New In Town…***

Salaam!

Wapendwa nachukua nafasi hii kuwakaribisha katika kazi yangu hii mpya ya fasihi.

Ni kitabu cha riwaya kiitwacho ***Bayo na Imbori (Ladha ya Jasho Tamu)***.

Kitabu kinamzungumzia msichana aitwaye Imbori kutoka Ayalabe, Manyara. Binti ambaye pamoja na kadhia mbalimbali alizopitia katika ukuaji wake anafanikiwa kutimiza ndoto yake ya kuwa wakili.

Imbori akifikiri baada ya kutimiza ndoto hiyo aliyoipambania kwa machozi na maumivu makali, amemaliza mapambano kwenye maisha yake na sasa ni wakati wa mchumia juani kulia kivulini, kumbe alijidanganya. Hekaheka zinaibuka katika sura mpya na mara hii inatokana na uadilifu aliokuwanao kwenye kazi zake za kusimamia haki.


Bayo ambaye ni binamu yake Imbori, akiwa mwanahabari anashindwa kujiweka mbali na maswaibu yanayompata nduguye.
Anaamua kutumia taaluma yake ya habari kupambana na udhalimu aliokuwa anatendewa nduguye; hapo ndipo kilichompata peku, ungo pia kinampata. Bayo naye moto unamuwakia.

Visa katika kitabu hiki vimesimuliwa kwa weledi mkubwa ambapo mbali na elimu vinatoa burudani kwa msomaji.

**Kitabu kinapatikana kwa Tsh. 13,000/.**
**Mawasiliano: simu ya mkononi 0685590548.**

**WhatsApp: https://whatsapp.com/biz/**
**Kwa Dar es Salaam unaletewa popote pale utakapokua.**
**Mikoani nauli ni Tsh. 8,000.**

*Karibuni sana.*



# KITABU: KIMBUNGA (DIWANI)

**JINA LA DIWANI : KIMBUNGA**

**MWANDISHI: HAJI GORA HAJI**

**MWAKA: 1995**

Katika safu yetu ya Pitio la Vitabu, toleo la 29 tunahama kutoka katika riwaya na kuangazia diwani (ushairi). Basi wale wapenzi wa tanzu ya ushairi, twende pamoja katika kuipitia diwani hii kama tulivoitoa katika mtandao.

---

**UTANGULIZI**

Kimbunga ni diwani inayozungumza juu ya mawaidha mbali mbali katika maisha pamoja na suala zima la ujenzi wa jamii mpya.Katika diwani hii,mwandishi ametoa maadili na maonyo mbali mbali pamoja na mbinu mbalimbali za kufuata ili kufanikiwa katika suala zima la ujenzi wa jamii mpya hapa nchini.

**MAUDHUI;**

**DHAMIRA KUU**-Ujenzi wa jamii mpya

Mwandishi amejadili dhamira ya ujenzi wa jamii mpya katika kazi yake.Mwandishi ameonesha vikwazo mbali mbali vinavyokwamisha ujenzi wa jamii mpya hapa nchini, Vikwazo hivyo ni kama vile uongozi mbaya, rushwa, tamaa, ukosefu wa elimu, ukoloni mamboleo, n.k.

Katika kujadili dhamira hii mwandishi ameonesha mbinu/njia mbalimbali ambazo jamii inapaswa kuzitumia katika suala zima la ujenzi wa jamii mpya hapa nchini,hizo ndizo dhamira ndogo ndogo;

**1. Uongozi Mbaya**

Mwandishi ameonesha kuwa Uongozi bora unahitajika kwa jamii yoyote ile ili kuleta ufanisi mzuri katika utendaji na utekelezaji wa majukumu mbalimbali kwani Uongozi mbaya unasababisha kushindwa kufikia malengo. Kutokana na uongozi mbaya ndiyo maana jamii hufikia kufanya mapinduzi ili kuuondoa uongozi uliopo na kusimika uongozi mpya ili kuijenga jamii kwa upya.

Katika shairi la "Kimbunga" (uk 1) mwandishi anaongelea juu ya mapinduzi yanayofanywa na tabaka la chini dhidi ya tabaka tawala. Mwandishi anasema;

*"kimbunga mji wa siyu, kilichowahi kufika,*


*Si kwa yule wala huyu, ilikuwa patashika,*

*Kimeing'owa mibuyu, minazi kunusurika,*

*Nyoyo zilifadhaika".*

Mwandishi ametumia mji wa Siyu kama kielelezo kizuri kwa jamii yeyote inayotaka kufanya mapinduzi ili kuondoa viongozi wabaya/wabovu na kuleta viongozi bora.Katika mapinduzi hayo mwandishi amefafanua kuwa wananchi wengi ndio wanaoathirika na wachache hunusurika.

Shairi la "Madanganyo" mwandishi anazungumzia jinsi uongozi mbaya unavyowadanganya wananchi na jinsi unavyowaathiri na kuwakera wananchi. Wananchi hushiriki katika shughuli za uzalishaji mali (miradi mblimbali) lakini matunda ya jasho lao huliwa na wachache. Wachache hao husahau wale waliosulubika katika uzalishaji na matokeo yake wananchi wanaishia kuishi maisha ya




taabu. Katika Ubeti wa 6, msanii/mwandishi anasema;

*"Mlitupigia mbiu, tulimeni ushirika,*

*Tukakatana miguu, kwa mapanga na mashoka,*

*Manufaa kwa wakuu, wadogo yetu mashaka,*

*Wezeni kutukumbuka, mjue nasi wenzenu."*

Shairi la "Wenye Vyao Watubana" mwandishi amejadili namna matajiri jinsi wanavyowagandamiza,kuwanyonya na kuwabana wale wasio na chochote yaani maskini.

***Itaendelea toleo lijalo***

# -SAIKOLOJIA-

## USIJITOTOSHE ILA USIACHE KUWA MNYENYEKEVU

**Neema Mbilinyi Mgao.**

**WhatsApp no. 0746-139654.**

**Dodoma.**



[Marudio—kwa wasomaji wapya]

Kwanza tuone maana ya maneno hayo mawili.

**Kujitotosha**

Hii ni ile hali ya kufanya mambo ya kitoto, ni ile hali ya kujiona hutoshi kwenye utekelezwaji wa jambo fulani. Waweza sema ni ile hali ambayo mtu hujionesha kuwa anaweza kufanya jambo fulani kwa uchache.

**Unyenyekevu**

Ni ile hali ya kuwa na heshima, ile hali ya kujali au ile hali ya kunyenyekea kwa watu. Ieleweke kuwa kunyenyekea sio kujishusha au kujidharaulisha. Bali ni kuonesha heshima.

Baada ya kuona maana ya maneno hayo basi sasa tuone ufanyaji kazi wake.

Kujitotosha, mara ngapi umesikia mtu akisema "jamaa ana mambo ya kitoto", yawezekana ni mara nyingi, lakini hapa tunaongelea ile hali ya kujifanya mtoto wakati kiuhalisia sio kweli. Sasa unakuta mtu amechaguliwa kuongoza mahali, anadhani kuwa ili aonekane anafaa basi anaanza kujitotosha, yaani anaanza kufanya mambo kwa kujishusha saana, sasa watu wamekuamini wamekupa jukumu la kuwaongoza, sasa kuanza kujitotosha ndo ili iwe na maana ipi? Jiamini fanya kazi kwa ukubwa ulioaminiwa.

Wengine wanadhani unyenyekevu ni kujifanya haujui, hapana. Unyenyekevu ni kuwa na nidhamu ya hali ya juu sana katika ufanyaji kazi wako. Unyenyekevu ni kuheshimu kila lika katika maisha yako, unyenyekevu sio kujitotosha.

Unyenyekevu sio kuomba omba msamaha wakati haujakosea, jiamini kwa kazi unayoifanya, katika jambo unalofanya, jiamini na ujikabidhi kwa Mungu, panga namna nzuri itakayokuridhisha katika kutekeleza majukumu yako ya kila siki, ukishajiandaa na kupanga mikakati ya kuwezesha kufanikisha basi fanya sasa jambo hilo kwa weledi. Sasa katika kulifanya jambo hilo, maadamu umeshalipangilia vizuri basi usijitotoshe bali uwe na nidhamu.

Usijitotoshe, wewe ni mtu mkubwa, na ndio maana ukakabidhiwa jukumu hilo, sasa ukijifanya uoneshe kuwa huwezi si unaona utawavunja moyo waliokuamini na kuamini kuwa unaweza kulifanya jambo kwa weledi. Ukijitotosha unawapa kazi kwanza ya kukufanya ujione unaweza, na unaweza ukawapa kuenda mbele zaidi ya wao kuhakikisha wanakufatilia kwenye utekelezaji wa majukumu yako.

Jiamini na jiaminishe katika shughuli zako, jiaminishe kwao kuwa wewe ni imara na unaweza kutekeleza majukumu yako bila usimamizi wala uangalizi wao. Watu wengi wanadhani kuwa ili wapendwe basi ni kujitotosha, yaani unakuta ni mtu mkubwa tuu lakini anafanya mambo ya hovyo hovyo tuu mpaka unaweza kudhani mtu ameruka hatua ya ukuaji. Jiamini wakikuamini, usijitotoshe. Unapojitotosha wanakudharau, utekelezwaji wa mambo mbalimbali unahitaji watu waliomakini ili kuimarisha mambo hayo, sasa ukijiweka kuwa wewe ni mtoto si unaona baadhi ya mambo yatakwama.jiamini fanya mambo kwa weledi na uzingativu.
Kisaikolojia, ile tabia unayoifanya mara kwa mara inakaa kichwani, sasa ikiwa unajidharau na kujitotosha basi utaonekana haufai, na ukizoea kujidharaulisha na unajidharau kweli na wanakudharau pia.

**Madhara ya kujitotosha.**

**1. Hawatokuamini.**
Utaona wanakuona una mambo ya kitoto hivyo wanaweza wakakutoa katika nafasi uliyopo. Hawatokuamini tena, sasa watamwaminije mtu asiyejiamini yeye mwenyewe, mtu anaejitotosha yaani anajiona hatoshi mahali fulani, huyo ataaminikaje, ni wazi kwamba imani itaondoka.

# -SAIKOLOJIA-

## USIJITOTOSHE ILA USIACHE KUWA MNYENYEKEVU

**2. Hawatokuheshimu.**
Sio tuu wataacha kukuamini, lakini pia hata heshima itaondoka, sasa utamheshimu vipi mtu ambae yeye hajiheshimu. Hawatokuheshimu kwa kuwa mpaka wanakupa usimamizi wa jambo fulani wewe ni wazi kuwa wamekuona unafaa. Sasa ukishaonesha hali ya kujitotosha ni dhahiri kuwa watakudharau. Anaheshimiwa mtu anaejiheshimisha, yeye mwenyewe anajidharaulisha ataheshimiwaje, hivyo jua kabisa ukijitotosha hawatokuheshimu.

**3.Watakutoa nafasi uliyopo.**
Ndio, watakutoa katika nafasi waliyoamini unaweza kufanya jambo. Sasa yanini kumpa mtu heshima ambapo yeye mwenyewe anajitotosha. Yaani yeye anajiona kuwa ni mtoto kutekeleza mambo mbalimbali sasa ni lazima atafutwe mtu aliye na maamuzi thabiti katika kuendesha mambo mbali mbali. Watakutoa thamani katika utekelezaji wa mambo yako.

Usijifanye haujui mambo ingawa inakupasa kujinyenyekeza sana, unyenyekevu katika kazi zako za kila siku ni jambo muhimu. Ila nyenyekea pale inapopaswa kunyenyekea, sio muda wote hata muda unaoona hili jambo ni hatari kwako eti umesimamia tuu kunyenyekea, hapana. Uwe imara na katika kunyenyekea uwe mtu wa kujiamini. Dunia inataka mtu makini anaejiamini hivyo usiruhusu watu kujua madhaifu yako. Bali watu waushuhudie uhodari wako muda wote, watu wakuone imara nyakati zote, watu wanahitaji kiongozi anaejiamini sana ili kuwaongoza vyema, hivyo ni muhimu kujiamini, kuwa na maamuzi imara na kuwa na utashi wa kufikiri mambo mbali mbali yatakayoleta tija katika maisha yako ya kila siku.

Usijitotoshe.






# HADITHI: NILIMUUA DADA NIOLEWE NA SHEMEJI-14



**Na. Makoleko Kalibonge**

***Ilipoishia,***
**Alisema mizimu ilimwambia pia kuwa, ili dawa zikubalike nilitakiwa kupeleka hizo shilingi kumi kumi bila kukosa ama kuchelewesha kila mwezi. Kuondoka kwangu kwenda Marekani itakuwa balaa kubwa.**

***Endelea,***

Nitakosa kupeleka kwa miezi miwili na haikutakiwa kulipa kwa mkupuo mmoja – kila mwezi ulijitegemea. Aliniambia kufika kwangu kila mwezi mbele ya mizimu ndiyo ilikuwa kafara yenyewe.
Nilipoambiwa hivyo nilichoka sana. Sikujua niliondokaje kwa mganga hadi nyumbani. Ingawa alinishauri nimwambie mume wangu jambo hili kwa nia njema lakini sikukubaliana naye. Nilibakiwa na miezi michache kukamilisha mtihani huu ili niyafurahie maisha. Sasa nlikutana na kizuizi kikubwa ambacho kitaniharibia kila kitu. Ama kwa hakika kisicho riziki hakiliki hata kama kimefika mdomoni.

Tangu siku hiyo nilikuwa mtu wa mawazo sana. Mume wangu alijtahidi kuwa karibu nami. aliniliwaza na kunifanya nijione wa pekee. Haikuwa rahisi. Hakulijua tatizo langu.

Siku ya safari ilifika. Tulijiandaa tukaondoka kuelekea Marekani. Bado sikuwa na amani ya moyo wala furaha ya maisha. Tukiwa Marekani, tulitembelea sehemu nyingi nzuri zenye kuvutia. Tulifanya manunuzi ya namna kwa namna. Mume wangu aliendelea na shughuli zake. Tulikutana na watu mbalimbali kutoka sehemu mbalimbali hasa ambao walikuwa marafiki wa shirika alilofanya kazi mume wangu. Miezi miwili ya kukaa huko ilikwisha. Tulifanyiwa mipango ya kurudi nyumbani Tanzania kuendelea na maisha.

Tulipofika nyumbani nilikuwa na wasiwasi mkubwa wa kukutana na vituko. Nilikuwa na tahadhari sana. Zilikatika siku tatu bila kukutana na kashkashi za aina yoyote. Kwa mwendo huo nilijipa matumaini ya kuendelea kuishi. Siku ya nne ilikuwa Jumatatu. Mume wangu alitakiwa kwenda kazini kupeleka taarifa ya safari yake. Asubuhi nilimuandaa kama kawaida na baada ya kufungua kinywa, aliondoka na gari lake kwenda kazini nami nilibaki nyumbani. Hapo ndipo mambo yalianza.

Mara tu mume wangu alipoondoka niliingia jikoni kuanza kufanya usafi. Nikiwa huko nilisikia kama kitu kimeangua sebuleni. Niliingiwa na woga. Wakati huo nilikuwa peke yangu. Mfanyakazi wa ndani alikuwa hajarudi sokoni. Nilitoka jikoni haraka nikajionee kulikoni huko sebuleni. Nilipofika nilikaribia kuzimia kwa mshtuko. Nilimkuta dada amekaa kwenye sofa akiwa amempakata mtoto mdogo wa kiume. Mtoto huyo alifanana sana mume wangu. Niliogopa sana. Zile kelele nilizozisikia ilikuwa chupa ya kunyonyea maziwa. Chupa hiyo alikuwa nayo mtoto ikamdondoka.

Ajabu! Dada aliponiona hakujishughulisha nami. aliendelea kumbembeleza mwanawe. Jambo lingine lililonishangaza ni mwonekano wa dada. Alikuwa nadhifu mno. Alipendeza mara dufu. Alikuwa amevalia nguo aliyokuwa nayo mara ya mwisho alipofikishwa Hospitali. Bado hakuonesha nia na mimi wala hakuwa na ulalamishi au kulia kama hapo awali. Aliendelea kumbembeleza mtoto hadi akalala.

Aliiinuka akiwa na mtoto amembeba mikononi akaingia chumbani kwetu ambako ni chumbani kwake kwa zamani. Muda mfupi baadaye alitoka akiwa mikono mitupu. Alikwenda kukaa palepale alipokuwa amekaa mara ya kwanza na mtoto. Nilisimama pale kwa dakika karibu ishirini. Msichana wa kazi aliporudi alinikuta nimesimama kama askari-mlinzi wa mwenge. Macho nimeyakodoa kuelekea kwenye sofa alipokaa dada.

“Dada vipi mbona uko hivyo?” Aliniuliza msichana wa kazi.
“Hakuna kitu mdogo wangu. Ingia tu huko jikoni ukaweke hivyo vitu,” nilimjibu. Macho yangu bado yaliendelea kuangalia kwenye sofa. Msichana wa kazi aliangalia nilipoelekeza macho kwa udadisi. Aliyatembeza haraka akayarudisha. Hakuona kitu. Dada aliendelea kukaa kwenye sofa. Alipotosheka aliingia chumbani akajifungia. Hamu ya kufanya kitu chochote ilipotea. Kila nilichopanga kukifanya siku hiyo sikukifanya. Nilibaki na mawazo lukuki. Nilijua yale niliyoelezwa na mganga yanatokea.

# HADITHI: NILIMUUA DADA NIOLEWE NA SHEMEJI—14

Kama ilianza hivi ilimaanisha mume wangu akirudi jioni atamuona. Akionekana na mume wangu ataonekana na kila mtu. Akishaonekana itakuwaje?

Siku hiyo nilishinda bila kula wala kufanya jambo lolote. Niliwaza na kuwazua. Niliogopa hata kuingia chumbani. Kila mara nilipenda kukaa na mfanyakazi. Nilijifanya kumuongelesha ili nisifikirie kitakachotokea jioni baada ya kufika mume wangu. Haikusaidia lakini angalau ilinifanya niwe *busy*. Ilipofika jioni mume wangu alirudi. Alinikuta kama alivyoniacha asubuhi. Hakuniuliza japo alishangaa, na pengine alidhani nilikuwa na kazi nyingi sana za kufanya. Miezi miwili haikuwa michache. Aliingia chumbani nami nikamfuata nyuma nyuma nikiwa na wasiwasi wa kumkuta dada. Tulipoingia chumbani hatukumkuta dada wala mtoto.

Nilishukuru nikashusha pumzi ndefu. Baadaye tuliingia bafuni kuoga. Tulipotoka huko tulijiandaa kwenda kwa mama na baba. Tangu tumerudi Marekani hatukwenda kuwaona. Tulipokwishajiandaa, tulitoka hadi nje ambako tulijipakia garini tayari kwa safari. Nilipoingia garini mume wangu aliliwasha tukaianza safari. Gari ilipoanza kuondoka nilihisi haja kubwa na ndogo zikitaka kunitoka kwa pamoja. Niligeuka nyuma kuangalia siti za katikati. Nguvu ziliniishia kabisa. Nilimuona dada amekaa akiwa amempakata mtoto. Mkao huo ulikuwa kama alivyokaa asubuhi sebuleni. Aliponiona hakushtuka. Ilionesha safari hii hakutaka kabisa kunilalamikia wala kunililia. Niliogopa sana huko tuendako itakuwaje. Sikusema kitu hadi tulipofika kwa mama. Dada alikuwa mtu wa kwanza kuteremka. Moja kwa moja aliingia ndani akiwa na mwanawe. Tulipoingia ndani nilimkuta amekaa jirani na mama akimnyonyesha mwanawe. Aliinua kichwa tukakutanisha macho. Alitabasamu. Niliwaangalia wenzangu kuona kama walimuona. Hakuna aliyemuona. Tulikaa kwa mama na hata ulipofika wakati wa kurudi nyumbani mambo yalikuwa yaleyale.

Usiku sikuwa na amani. Usingizi ulipaa. Nililala dakika tano nikawa macho muda mrefu. Shida hiyo ilinifanya nikate shauri kesho yake niende Bagamoyo nikamueleze mganga ajue namna ya kunisaidia. Japo nilijua ilikuwa ngumu sana sikuwa na njia nyingine.

Kulipopambazuka nilimuandaa mume wangu kama ilivyo ada. Baada ya kufungua kinywa aliondoka kuelekea kazini kwake. Alipoondoka nikafanya jitihada nami nikajiandaa kisha nilimuachia maagizo mfanyakazi. Niliwambia nakwenda kumuangalia rafiki yake dada ambaye alikuwa anaumwa. Hivyo, kama nitachelewa kurudi aandae chakula cha jioni. Nilipomuachia maagizo hayo nilichukua mkoba wangu nikaupachika begani nikatoka.

Nilipoufika mlango wa mbele ili nitoke nje nilikutana na dada amesimama katikati ya mlango. Nilipiga kelele kwa nguvu hata mfanyakazi alikuja mbio.
“Vipi dada?” Aliniuliza.
“Nilitaka kuanguka,” nilimwambia.
“Pole.”
“Asante. Nenda kaendelee na kazi zako.” Yule msichana aliondoka. Aliniacha niliposimama huku nikitazamana na dada. Baada ya kusimama kwa muda dada alitoka mlangoni huku akicheka sana. Kicheko chake hakikuwa cha kawaida. Hakikuashiria furaha wala huzuni. Labda kilikuwa cha bezo. Nilipohakikisha ametoka nilipita mbio. Kicheko cha dada kikiendelea kuhanikiza nyuma yangu. Sikutaka hata kugeuka nyuma.

Moja kwa moja hadi kituo cha daladala ambako nilipanda gari hadi Mwenge halafu gari jingine hadi Bagamoyo. Nilipoteremka stendi moja kwa moja hadi nyumbani kwa mganga. Nilipofika nyumbani kwa mganga nilistaajabu kuona sura ngeni nyingi. Pia sikuona dalili ya kuwa na mganga karibu. Ilikuwa kama amesafiri basi ana muda mrefu tangu aondoke. Hapakuwa na dalili ya kurejea karibuni. Kiroho kilianza kunidunda taratibu halafu kikanidunda kwa kasi na kijasho chembamba kilianza kunitoka.

“Karibu dada.” Ilikuwa sauti ya kaka mmoja aliyenishangaa.
“Asante. Nina shida na mtaalamu.” Niliitikia makaribisho yake nami nikaeleza shida yangu.

“Mtaalamu yupi tena?” Badala ya kunijibu aliniuliza swali. Alinichanganya hata nikadhani nimekosea sehemu husika. Niligeukageuka mara kadhaa kuangalia mazingira ya pale. Nilijiridhisha kuwa sijakosea. Nilikuwa sehemu sahihi.

***Nini kitaendelea?***



**Muammar Abu Minyar Al Gaddafi**

**Alisoma kwa moyo mkunjufu mada za Nasser na Mapinduzi ya Ufaransa ya 1789, pamoja na kazi za mwananadharia wa kisiasa wa Syria Michel Aflaq na wasifu wa Abraham Lincoln, Sun Yat-sen, na Mustafa Kemal Atatürk.**

**Mafunzo ya kijeshi: 1963-1966**

Gaddafi alisoma historia kwa ufupi katika Chuo Kikuu cha Libya huko Benghazi kabla ya kuacha na kujiunga na jeshi. Licha ya rekodi yake ya polisi, mnamo 1963 alianza mafunzo katika Chuo cha Kijeshi cha Kifalme, Benghazi, pamoja na marafiki kadhaa wenye nia moja kutoka Misrata. Majeshi ya kijeshi yalitoa fursa pekee kwa ajili ya kusonga mbele kwa jamii ya Walibya wasiojiweza, na Gaddafi aliitambua kama chombo kinachowezekana cha mabadiliko ya kisiasa. [Chini ya Idris, wanajeshi wa Libya walipewa mafunzo na jeshi la Uingereza; hili lilimkasirisha Gaddafi, ambaye aliwaona Waingereza kama mabeberu, na kwa hiyo, alikataa kujifunza Kiingereza na akawakosea adabu maafisa wa Uingereza, na hatimaye kushindwa mitihani yake. Wakufunzi wa Uingereza walimripoti kwa ukaidi na tabia ya unyanyasaji, wakimtuhumu kwamba alihusika katika mauaji ya kamanda wa chuo cha kijeshi mwaka wa 1963. Ripoti kama hizo zilipuuzwa, na Gaddafi akaendelea katika kozi hiyo.

Akiwa na kundi la makada waaminifu, mwaka 1964 Gaddafi alianzisha Kamati Kuu ya Harakati Huru ya Maafisa, kikundi cha mapinduzi kilichopewa jina la mtangulizi wa Nasser wa Misri. Wakiongozwa na Gaddafi, walikutana kwa siri na kupangwa katika mfumo wa seli za siri, wakiweka mishahara yao pamoja. Gaddafi alizunguka Libya akikusanya taarifa za kijasusi na kuendeleza uhusiano na watu wanaomhurumia, lakini idara za kijasusi za serikali zilimpuuza, zikimchukulia kuwa tishio kidogo. Alipohitimu Agosti 1965, Gaddafi akawa afisa wa mawasiliano katika kikosi cha ishara cha jeshi.

Mnamo Aprili 1966, alitumwa Uingereza kwa mafunzo zaidi; kwa zaidi ya miezi tisa alipitia kozi ya lugha ya Kiingereza huko Beaconsfield, Buckinghamshire, kozi ya wakufunzi wa mawimbi ya Jeshi la Air Corps katika Kambi ya Bovington, Dorset, na kozi ya wakufunzi wa jeshi la ardhini huko Hythe, Kent. Licha ya uvumi wa baadaye kuwa kinyume chake, hakuhudhuria Chuo cha Kijeshi cha Kifalme Sandhurst. Mkurugenzi wa kozi ya ishara ya Bovington aliripoti kwamba Gaddafi alifanikiwa kushinda matatizo ya kujifunza Kiingereza, kwa kuonyesha amri thabiti ya utaratibu wa sauti. Akigundua kwamba mambo ya Gaddafi aliyopenda sana yalikuwa kusoma na kucheza kandanda, alimdhani kuwa "afisa mcheshi, mchangamfu kila wakati, mchapakazi na mwangalifu". Gaddafi hakuipenda Uingereza, akidai maafisa wa Jeshi la Uingereza walimtusi kibaguzi na kupata ugumu wa kuzoea utamaduni wa nchi hiyo; akithibitisha utambulisho wake wa Kiarabu huko London, alitembea karibu na Piccadilly akiwa amevaa mavazi ya kitamaduni ya Libya.

Baadaye alisimulia kwamba alipokuwa akisafiri kwenda Uingereza akiamini kuwa ni ya juu zaidi kuliko Libya, alirudi nyumbani "akiwa na imani zaidi na fahari juu ya maadili yetu, maadili na tabia yetu asilia". ***Itaendelea..***

# SAKO KWA BAKO:
## Eva Mrema: MWANAMKE MWENYE THAMANI NDANI YANGU

**Juma hili, siku ya jumamosi katika Hoteli ya Golden Tulip, jijini Dar es salaam, palifanyika tukio kubwa la uzinduzi wa kitabu 'MWANAMKE WA THAMANI NDANI YANGU' cha mwandishi Eva Mrema. Ngurumo ya Mwandishi lilivutwa na tukio hilo na hata kumtafuta mwandishi huyo sako kwa bako aweze kutueleza machache tu katika hilo. Huyu hapa Da' Eva…**

**Kwanini kimezinduliwa MWANAMKE WA THAMANI NDANI YANGU na si kile cha KUNGWI?**
Mwanamke wa thamani ndani yangu ni maono juu ya maarifa anayoyahitaji mwanamke ili kuwa bora.
Kwangu ni kitabu mama huku KUNGWI ni mtoto wake.

Ndani ya Mwanamke Wa Thamani kuna kujitambua, kujua kusudi na kuelewa aina ya maisha anayopaswa kuishi mwanamke. Ilhali ndani ya Kungwi kuna mafundo, usafi binafsi na mazingira, usafi wa mwenza na mambo muhimu kuhusu ndoa.

Hauwezi kuruka hatua. Mwili wenye afya unaihitaji sana roho iliyotulia. Kwenye hivi vitabu viwili.... MWANAMKE WA THAMANI NDANI YANGU ni roho na KUNGWI ni mwili.
Nimeizindua roho ya maarifa ya mwanamke.

**Hebu tueleze kwa ujumla, ilikuwaje mpaka kufikia hatua ya kuzindua kitabu chako.**

Kitabu cha mwanamke wa thamani ndani yangu niliandika mwanzoni mwa mwaka 2023.
Nilianza rasmi kukifikisha kwa hadhira mwaka huo huo mwezi wa tano.
Kimepitiwa na kusomwa na waaandishi na baadhi ya watu wenye weledi katika tasnia ya uandishi.
Nimekiboresha zaidi ya mara tatu na mwisho kabisa nimekiboresha mwaka huu 2024 mwezi wa kwanza.
Mpango wa kuzindua nilikuwa nao tangu siku ya kwanza kukitoa ila kwa sababu za kiuchumi na nafasi, sikufanikiwa.

Safari ya kukizindua imeanzia kwa mama Ailinda Sawe, Mke wa mwandishi nguli, baba wa fasihi, Mwafrika Merinyo. Mama Ailinda alinikutanisha na mama mwingine, Asma Makau, mmoja wa wakurugenzi wa STARA TANZANIA...




Kwa upendo wa ajabu, usio na masharti nikapata udhamini wa kufanya uzinduzi.

Uzinduzi rasmi wa kitabu cha MWANAMKE WA THAMANI NDANI YANGU umefanyika kwa mafanikio makubwa tarehe 24/2/2024.
Tukio lilifanyika katika Hoteli ya Golden tulip, iliyopo eneo la Posta Jijini Dar es salaam. Shukrani kwa kila mkono uliojitoa kufanikisha hili.

**Ok! Si vibaya kutujuza ni vipi na wapi twaweza kupata vitabu hivi…**
Vitabu hivi vinapatikana kwa mtindo wa nakala laini .. (softcopy) kwa shilingi za kitanzania 5000 kwa kimoja.
Nakala ngumu (hard copy) kwa shilingi za kitanzania 10,000 kwa kimoja.
Karibu sana ujibatie vitabu vilivyosheheni maarifa adhimu kwa mwanamke.
Nipigie au nitumie ujumbe WhatsApp. No +255742630141 nitakusikiliza.

**Ngurumo ya Mwandishi, twakutakia kila la kheri.**

# UNAYE RAFIKI?



**Mtunzi: Salum Makamba**

"Mwanagenzi"
Katika kijiji cha Mnyakweupe kulikuwa na shule yenye wanafunzi wa vidato mbalimbali. Katika moja ya kidato kulikuwa na darasa lenye mwanafunzi wa kike aliyekuwa na tabia ya ajabu. Kuuliza maswali mengi kupita kiasi katika kila kipindi.

Tabia hiyo ilikuwa inawakarahisha sana wanafunzi wenzake pamoja na baadhi ya walimu lakini katu hakuiacha. Wengi walikuwa wakiamini kwamba mwanafunzi huyo ni juha ndiyo maana anauliza maswali mengi ili aweze kuelewa. Lakini kuna jambo likawa linawafanya watilie mashaka mtazamo wao huo. Mwanafunzi wanayemdhania kuwa ni juha kila wanapofanya mtihani basi yeye ndiye anaibuka kinara. Ikawa kila mmoja anajiuliza, "Inawezekanaje anaongoza kwa ufaulu ilhali wakati wa vipindi huwa haoneshi kuelewa zaidi ya kuuliza maswali mengi tena mengine yasiyo na maana?"

Hakuna aliyeweza kung'amua. Baadhi ya wanafunzi wenye chuki walizusha kwamba lazima atakuwa anatumia mbinu za udanganyifu wakati wa mitihani ndiyo maana anafaulu. Maneno hayo yaliwafikia walimu ambao walichukua jukumu la kumwekea mitego binti huyo. Lakini hawakufanikiwa kumkamata hata mara moja akitumia njia za udanganyifu. Siku moja Kiranja wa Taaluma aliamua kumfuata binti huyo na kumuuliza anawezaje kufaulu kwa alama za juu ilhali darasani huwa anaonesha ni mwenye kusuasua katika uelewa kutokana na aina ya maswali ambayo huwa anauliza.

Binti alimtazama Kiranja wa Taaluma kisha akamuuliza, "Kwa nini unataka kufahamu?"
Kiranja wa Taaluma akajibu, "Kwa sababu huwa sipendezwi na namna unavyokaripiwa na wakati mwingine kudhalilishwa kutokana na maswali yako darasani labda naweza kupata njia ya kukusaidia ili usiwe unayauliza."
Binti alitabasamu kisha akamtupia swali Kiranja wa Taaluma, "Unamjua Chaupole?"

Kiranja wa Taaluma akaitikia ndiyo huku akitikisa kichwa kukubali kisha akaongeza, "Si yule rafiki yako ambaye huwa mnapenda kuongozana muda mwingi kama tetea na mwanawe?"
Binti naye akatikisa kichwa kumkubalia Kiranja wa Taaluma kisha akamwambia, "Basi ni mwoga sana wa kuuliza maswali darasani. Yaani hata kama hajaelewa basi hawezi kunyoosha kidole ili aulize."

"Enhe!" Kiranja wa Taaluma alionesha shauku.
Binti akaendelea kueleza, "Sasa kutokana na hali hiyo mimi nimechukua jukumu la kuwa nauliza kila swali lake. Nina uwezo wa kuwa namwelesha lakini huwa nataka apate majibu kutoka kwa mwalimu wa somo husika."
"Aisee! Na umekuwa tayari kudharauliwa, kulaumiwa na kupachikwa majina mabaya yote kwa ajili ya rafiki yako tu?"
Binti alikubali kwa kutikisa kichwa kisha akasema, "Kama ilivyo vema marafiki kuwa wamoja wakati wa fanaka basi yapaswa ibaki vivyohivyo na kwenye nakama."

Kiranja wa Taaluma alitikisa kichwa kisha akaondoka akiwa amepata funzo kubwa. Mtu yupo tayari kudhalilika ili kumsaidia rafiki yake pamoja na kumfichia aibu zake. Akajiuliza wakati anatembea, "Je ninaye rafiki wa namna hiyo?" Ubongo wake ukazama

kwenye tafakuri. Chambilecho mwanamasumbwi Muhammad Ali, “Urafiki ni jambo gumu mno kulielezea duniani. Siyo jambo unalofundishwa shuleni. Lakini kama hautajifunza maana yake basi kwa hakika hakuna ulichojifunza maishani.”

Je, wewe unaye rafiki aliye tayari kudhalilika ili kukustiri? Jitathmini!

**Mwisho**

KITABU MAISHA
Ni shirika lisilo la kiserikali lenye ofisi zake mjini Iringa, lililosajiriwa kwa namba 00NGO/R/4382.

Lengo kuu la shirika hili ni kujenga na kukuza utamaduni wa kusoma vitabu katika jamii kwa kuanzisha vilabu vya usomaji vitabu kuanzia ngazi za shule za sekindari nchini na mitaani. Pia kuwa na mradi wa ‘book box’ kwa shule za msingi.

Je wapenda kuwa mmoja wa wadau katika mbio hizi?

Tunaomba utuchangie kitabu kimoja au hata zaidi ili kuweza kufikia lengo letu lwa mwaka 2024 ambapo tunahitaji vitabu 600. waweza kutupatia/kutununulia kipya au kutuchangia pesa taslimu kiasi chochote ulichojaaliwa.

Kwa michango ya pesa tuma kwenda Tigo Lipa Namba 17120305 KITABU MAISHA.

Na kwa wale wanaopenda kutuchangia vitabu wasiliana nasi kwa simu namba 0674762549 / 0734550514. tunatanguliza shukrani zetu.






**"Mi nasubiri tu mniambie cha kufanya, kama tafutishi mnazo za kutosha, iliyobaki hapo ni kuanza matembezi kuona ukweli wa hivi vilivyopo na kupata mengine mengi kisha tutajua tunafanyaje," akamwambia.**

**"Ok, nimekuelewa kijana wangu, sasa kila mmoja ana jukumu lake juu ya hii kitu, na wewe nataka nikupe jukumu lako…"**
**"Sawa!"**

---

"Ingia kazini, peleleza kwa mikono na miguu kisha niletee jibu sahihi kwa njia yetu ileile ya siku zote ya kumaliza mambo," Madam alimwambia Amata. "Hilo ndilo nilikuwa nalisubiri sio kuweka siasa nyiiiingi… kuna mambo hayaitaji siasa kabisa hapa duniani," akajibu huku akisimama, "tegemea majibu kuanzia jioni ya leo," akamalizia huku akijitupia koti lake mwilini na kutoka mle ofisini.


⚜

Mara tu alipoiacha ofisi ya Madm S pale shamba, Amata akaelekea katika makao makuu ya maaskofu. Akaegesha gari lake na kuhakikisha milango imefungwa barabara, akavuta hatua mpaka kwenye mgahawa wa kisasa uliojengwa katika kituo hicho, akaketi mezani, punde si punde mhudumu wa mgahawa huo alimsogelea tayari kwa kumhudumia.

"Ugali samaki na bia moja baridi," akaagiza. Haikuchukua muda mrefu aliletewa na kuendelea kula. Alipomaliza na yule mhududmu akaja kuondoa vyombo ndipo alipomchokoza kwa maswali ya kutega.
"Samahani, kuna padre namtafuta, mzungu amekuja hapa siku hizi mbili…"
"Aaa Father Bibliot?" akadakiza.
"Ndiyo, huyo huyo, nahitaji kuonana naye alinambia nitamkuta hapa lakini simuoni, unajua chumba chake?" akauliza.
"Yeah, amefikia kule Vatican Wing, namba 304," akajibiwa. Amata akanyanyuka na kumuaga.
"Chenji yako bro'!"
"Keep it!" akamjibu akiwa na maana akae nayo kama zawadi yake. Amata aliingia katika jengo hilo kubwa lililokuwa na vyumba vingi. Alipofika mapokezi hakuona mtu yeyote.

"Thank God", akajisemea.
Maana kuna maeneo kuingia ni ishu hata uwe mjanja vipi, akawaza huku akizipanda ngazi kuelekea ghorofa ya juu.
Mlango uliobandikwa namba hizo alizotajiwa aliuona kwa uwazi tu bila ya kificho chochote. Akauendea na kusimama mbele yake, akatega sikio na kuzima kelele zote kichwani mwake. Hakuna mtu! Akachomoa funguo yake isiyoshindwa kitu, mizungusho miwili tu kitasa kikatii, akazama ndani na kuufunga mlango. Chumba tupu, mezani kulikuwa na msalaba na vitabu kadhaa, hakugusa kitu, alitulia palepale na kuibonyeza saa yake mahali fulani, hakuna kilichotokea.

Clear, akili yake ikamwambia. Akavuta hatua kuiendea ile meza. Akatazama zile droo zilivyojipanga, akaingiza mkono mfukoni na kutoa gloves akazivaa.
Droo ya kwanza, hakuna cha maana, ya pili vilevile, ya tatu alkadhalika. Akatulia kidogo, akatoka na kuliendea kabati, akafungua na kukuta begi dogo lenye nguo na vifaa fulani fulani ambavyo yeye aliviielewa.




Mh! Kasisi gani huyu ana vifaa vya kijasusi namna hii! Akaingiwa shaka. Katika pekua pekua hiyo ya kiufundi zaidi, akakutana na kitabu cha kumbukumbu. Akapekua harakaharaka aone kama kuna lolote la kumfaa, hakuna, alipotaka kufunga kile kitabu jicho lake likavutiwa na maandishi fulani.

*…Secure Cronoc 7, meet me to the Dom at shone…*

Cronoc 7, Amata akawaza, hakujua hata maana yake nini. Ah! Mambo yao hayo wanayaelewa wenyewe, akaondoka taratibu kutoka katika chumba hicho, akateremka ngazi na kuibukia mapokezi ambako alikutana uso kwa uso na mhudumu wa afisi hiyo.
"Kaka, unatoka wapi?" akauliza yule mhudumu.
"Oh, samahani, mimi ni mgeni wa Bibliot, nilifika sikukukuta na nilikuwa na haraka sana, lakini bahati mbaya naye hayupo, sijui…"
"Uwe unasubiri, hii siyo hoteli kama hizo za mitaani kaka yangu, sawa?"
"Sawa dada," Amata akajibu kwa

unyenyekevu ambao nashindwa kuuelezea.
"We ndiye Carlos?" yule dada akauliza. Akili ya Amata ikafanya kazi haraka sana.
"Ndiyo mimi dada yangu," akajibu.
"Aliniachia ujumbe wako hapa!" akamwambia huku akichukua kitu fulani kwenye droo yake. Ilikuwa bahasha kubwa yenye ukubwa wa A4, lakini hii ilikuwa ngumu tofauti na zile tulizozizoea,
"Alisema ukifika nikupe," akamalizia na kukabidhi ile bahasha kwa Amata.
"Asante sana, sasa nina amani," Amata akajibu na kuondoka zake huku akimwachia yule dada shilingi elfu kumi kama zawadi.

Mara tu baada ya Amata kuondoka katika eneo lile, gari jingine jekundu likaegeshwa eneo lilelile alilotoka. Kijana mmoja mrefu akateremka akiwa ndani ya suti safi, akavuta hatua mpaka katika lile jengo kubwa lililojulikana kama Vatican Wing, akaingia na moja kwa moja akafikia mapokezi.

"Carlos Zejac!" akajitambulisha.

"Karibu sana,"

"Nimeambiwa kuna mzigo wangu hapa kutoka kwa Bibliot," akamwambia mara tu baada ya kusalaimiana na mwanadada huyo. Yule mwanadada hakujibu kitu akabaki kumwangalia yule kijana.

"Mi mbona siwaelewi kaka yangu!" akamwambia.

"Kivipi?"

"Hata nusu saa haijaisha ametoka Carlos na kachukua huo mzigo. Sasa we ni Carlos yupi tena?" yule mwanadada akajieleza. Carlos halisi, akabaki kapigwa na butwaa.

"Hapana, mimi ndiye Carlos, sasa huo mzigo umempa mtu mwingine. Dah!" akang'aka huku akizunguka huku na kule. Kijana huyo alichanganyikiwa alikadhalika na yule dada naye aliishiwa nguvu akajitupa kochini.

"Umefanya mistake kubwa sana ambayo italeta taabu, ah! Unamkumbuka huyo kijana?"

"Nikimwona nitamkumbuka,"

"Katoka muda mrefu?"

"Hapana yaani si ajabu mmepishana nje ya geti tu," yule mwanadada akajibu.

Carlos, akajaribu kurudisha mawazo nyuma akakumbuka kuwa kapishana na Lexus nyeusi ambayo ilitangulia kutoka getini kabla ya yeye kuingia ndani. Akatoka haraka kwenye ile ofisi na kukimbilia getini kwa walinzi.

"Samahani kuna jamaa katoka na Lexus nyeusi hapa…"

"Ndiyo, ndiyo, vipi kwani?" mmoja wa wale walinzi akauliza.

"Aaaann! kuna mzigo kauchukua kimakosa sio wa kwake, ni wa kwangu," akajieleza. Yule mlinzi akachukua kitabu chake cha usajili wa wageni na kupekua.

"Anaitwa Mr. Spark," kisha akamtajia na namba za simu ambazo yule kijana alizinakili, akabofya na kuiweka sikioni.

"Mteja unayempigia hapatikani kwa sasa…" ile simu ikamjibu. Carlos akachukizwa na jibu hilo, akalalama njia nzima akienda huku na kurudi. Akabofya namba nyingine na kuongea lugha ambayo hakuna aliyeielewa, alipomaliza akarudi zake kule mapokezi.

"Sasa dada mi naondoka lakini nitarudi baadae huyu bwana atakapokuwa amefika, itabidi wewe utusaidie kupata ile bahasha maana ni nyaraka za siri…" akamaliza na kuondoka zake akiwa amevimba kwa hasira.

Yule mwanadada akashusha pumzi ndefu, kifua chake kilikuwa kikitiririkwa na jasho jepesi, lililopita katikati ya matiti yake huku kikipanda na kushuka kwa hofu.
Nimelikoroga, mbona nitalinywa! Akawaza na kuinuka pale alipoketi lakini akajikuta hana nguvu kabisa, akajiegemeza ukutani, mawazo yakamfunika kama wingu la mvua, amani ikampotea na hofu kuu ikauvaa mwili wake.

Kamanda Amata aliegesha gari lake jirani kabisa na Viwanja vya Gym Khana, eneo ambalo lilikuwa tulivu, hakuna watu isipokuwa wale tu waliokuwa wakifanya mazoezi hasa vijana wa Kihindi. Akaichukua ile bahasha na kuiondoa pini iliyowekwa kwenye mfuniko wake. Ndani ya bahasha ile kulikuwa na karatasi kadhaa zilizochapwa kwa mashine, akazivuta nje. Zilikuwa zimefungwa vizuri na kubanwa kama kitini, safi. ***Itaendelea...***

**Kitabu cha CRONOC 7—chapa ya pili kitakuwa madukani muda wowote kutoka sasa.**

**Weka oda yako sasa kwa kutuandikia whatsapp 0766974865.**

**Na ukipenda kulipia kabisa waweza fanya hivyo kwa kutuma pesa '12,000/=' kwenda Mpesa Lipa Namba 5559006 JAMVI LA SIMULIZI kisha tutumie meseji ya muamala wako kwa whatsapp hiyo hapo juu.**

# Ya Kale Ni Dhahabu– Alibaba na Wezi 40 (7)

Alijaza dhahabu kwa punda wawili kisha akazifunika na kuni kisha akasema neno la siri la kufungia pango, "Fungaaaaa sesmiii!!!" na kisha akaondoka.

Alipofika nyumbani, mkewe Alibaba alikuwa akimsubiria. "Kaka yangu amekufa," Alisema Alibaba. "Nataka niupeleke mwili wake kwa mkewe sasa hivi."

"Oooh masikiti Kassim, kimetokea nini huko?" Alisema mke wa Alibaba. "aliweza kwenda pangoni na kuchukua dhahabu?"

"Alikwenda pangoni," alisema Alibaba. "lakini aliuliwa. Nafikiri wezi waliwahi kurudi na kumkamata. Walimuua kwasababu alitaka kuiba mali zao."

"Oooh masikini," alisema mke wa Alibaba. "lakini alitaka dhahabu kidogo tu, na hiyo imemgharimu maisha yake."

"Usimwambie mtu yeyote kuhusu hili," alisema Alibaba. "Sasa wacha mimi niupeleke mwili wa Kassim kwa mkewe, lakini, wakati mimi nimeondoka, chukua hizi dhahabu nilizokuja nazo na uzifukie pamoja na zile zingine."

Mke wa Alibaba akachukua dhahabu na jembe tayari kwa kwenda kuzifukia, na huku alibaba alimchukua yule punda alioubeba mwili wa kaka yake na kwenda kwa mkewe. Alibaba alipofika mlangoni kwa nyumba ya Kassim akagonga mlango, mfanyakazi wa Kassim aitwae Marjane akaja kumfungulia. Alibaba alimtazama Marjane kwa hali ya kuwa na matumaini fulani kwasababu alikuwa ni msichana muaminifu sana na alimuamini sana.

Marjane alipouona mwili wa bosi wake, ghafla akanyanyua mikono mpaka mdomoni na akatumbua macho kwa mshtuko na hofu.

"Kassim alikwenda msituni kwenda kuchukua dhahabu" alisema Alibaba kumwambia Marjane, "na dhahabu zile ni za wezi ambao walimfuma Kassim pangoni na kumuua."

"ila nina wazo" aliendelea kusema Alibaba, "nitauficha mwili huu kwenye ghala chini, halafu tutasingizia kwamba Kassim anaumwa na ameamua kupumzika chumbani kwake. Halafu baada ya siku tatu tutasema kwamba Kassim amefariki kutokana na ugonjwa.



Sasa nenda ukamwambie bosi wako (mke wa Kassim) kuhusu habari hizi mbaya. Ila usimwambie mtu yeyote mwingine kuhusu jambo hili."

Alibaba akauficha mwili wa Kassim katika ghala kisha akarudi kwenye kijumba chake kidogo.

"Sasa Kassim ameshafariki" Alibaba alimwambia mkewe, "mke wa kassim hatataka kuishi peke yake. Nafikiri bora tuhame hapa twende tukaishi kwake na tuondoke na dhahabu zetu zote. Pia, nyumba ya Kassim ni kubwa kuliko hii yetu. Na Marjane mfanyakazi wake atatusaidia kazi sote pamoja na tutamlipa dhahabu kidogo."

Hivyo basi, ilipofika jioni, Alibaba, mkewe na mtoto wao aitwae Khalid walihama na vitu vyao vyote mpaka kwenye nyumba ya Kassim. Ilipofika usiku, Alibaba akarudi kule nyumbani kwake kwa zamani na kufukua zile dhahabu kisha kwa siri akazipeleka kwenye makazi yao mapya.

Asubuhi ya siku iliyofuata, Marjane msichana wa kazi akaenda kwenye duka la dawa. Duka lilikuwa limejaa watu wengi wa mjini pale. Marjane kwa makusudi akaongea kwa nguvu ili kuhakikisha kila aliye pale anasikia.

"Nahitaji msaada wako!!" alisema Marjane kwa kulia, "anaumwa sana!!! Naomba nipatie vidonge ili nikampatie aweze kupata nafuu!"

Muuza duka alikuwa akitengeneza dawa, kamuangalia Marjane. "Nani anaumwa - Na nini kinamsumbua zaidi?" Aliuliza muuza dawa.

"Ni bosi wangu, Kassim. Anaumwa sana," Marjane alijibu huku akitokwa na machozi. "hawezi kula wala kuongea na anapata maumivu makali sana. Unaweza kunipatia vidonge tafadhali?"

Muuza duka akachukua chupa ndogo iliyokuwa na vidonge vyeupe kisha akampatia Marjane. " hizi zitampa nafuu, mpe vidonge viwili kila baada ya saa mbili."

"Ahsante sana!" alisema Marjane. Kisha akaenda nyumbani na kusubiri.

***Itaendelea...***

**Na. Richard Mwambe**

Mzee Ally Hassan Mwinyi alizaliwa Kivure kwenye Mkoa wa Pwani wa Tanzania bara lakini wazazi wake walihamia Unguja alipokuwa mdogo. Kuanzia mwaka 1933 alipata elimu ya msingi na sekondari kwenye shule za Mangapwani na Sekondari ya Dole alikohitimu mwaka 1942. Baada ya masomo ya ualimu aliendelea na elimu ya juu kwenye Chuo Kikuu cha Durham nchini Uingereza.

Alianza kufundisha shule huko Mangapwani na baadae akaendelea kuwa mkuu wa chuo cha ualimu Unguja hadi kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa wizara ya elimu ya Zanzibar baada ya mapinduzi mwaka 1963. Mnamo 1970 alipewa uwaziri wa nchi katika ofisi ya rais akaendelea na vyeo mbalimbali katika serikali ya Zanzibar, pamoja na uwaziri wa afya, wa mambo ya ndani na wa utalii. Alihudumia pia miaka mitano kama balozi wa Tanzania nchini Misri.

- **Mzee Ally Hassan Mwinyi (8 Mei, 1925—29 Februari, 2024)**
- **Rais wa tatu wa Zanzibar 1984**
- **Rais wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1985**



# KWAHERI MZEE ALLY HASSAN MWINYI

Januari 1984 aliteuliwa kuwa rais wa Zanzibar baada ya mtangulizi wake Aboud Jumbe Mwinyi kulazimishwa kujiuzulu. Katika nafasi kama rais wa Zanzibar alikuwa pia makamu wa rais wa maungano; katika uchaguzi wa 1985 aliteuliwa na CCM kuwa mgombea kwa nafasi ya uraisi wa muungano akachaguliwa bila mpinzani katika mfumo wa chama kimoja.

Wakati wa urais wa Muungano kwa Mwinyi, sera za Ujamaa zilianza kugeuzwa. Badala yake sera za soko huria zilianzishwa, masharti ya kuingiza bidhaa kutoka nchi za nje yalipunguzwa na uanzishaji wa biashara ya watu binafsi ulihamasishwa. Mwaka wa 1991, Mwinyi alianzisha Tume ya Nyalali iliyopendekeza kuanzisha mfumo wa vyama vingi nchini.

Wakati wa awamu yake kwenye mwaka 1995 ulitokea uchaguzi wa kwanza wa vyama vingi vya kisiasa nchini Tanzania.

Sera za soko huria za Mwinyi zimeendelezwa chini ya Rais Benjamin Mkapa. Mwinyi mwenyewe, baada ya kustaafu, hakujiingiza katika mambo ya siasa tena. Aliendelea kuishi nyumbani kwake huko Dar es Salaam.

Mzee Ally Hassan Mwinyi aliyekuwa na umri wa miaka 99 mpaka umauti unamkuta alitibiwa huko London miezi michache kabla ya kurudi nchini na kuwepo katika hospitali ya Emilio Mzena kwa uangalizi zaidi. Taarifa zinaeleza kwamba Mzee Mwinyi alikuwa akisumbuliwa na Kansa ya Mapafu.

Mnamo tarehe 29/2/2024, Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan alilitangazia taifa juu ya kifo cha Mzee Mwinyi.

Katika uhai wake, Mzee Mwinyi alitunukiwa Nishani ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mnamo mwaka 2011. mwaka 2012 alitunukiwa Shahada ya Uzamivu ya Heshima ya Udaktari wa Barua ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Na mwaka 2013 Chuo Kikuu Cha Afrika Mashariki kilimtunuku Udaktari wa Usimamizi wa Biashara.

Taifa limempoteza Mswahili mahiri aliyekijua na kukienzi Kiswahili siku zote za uhai wake.  Kila nafsi itaonja mauti. Upumzike kwa amani Baba Mwinyi.

# SHUBAKA LA VITABU

**Katika Safu yetu ya SHUBAKA LA VITABU leo tutawaletea Maktaba kumi (10) bora duniani. Je; wazijua hizo. Karibu uwe nasi upate kujua haya,**

## 9. MAKTABA YA KIFALME YA DENMARK

Ni muunganisho wa maktaba mbili za awali za kitaifa nchini Denmark: Maktaba ya Jimbo na Chuo Kikuu huko Aarhus na Maktaba ya Kifalme huko Copenhagen. Ingawa sasa ipo chini ya shirika moja, na maeneo tofauti katika miji yote miwili. Muunganisho huo ulianza kutumika Januari 1, 2017.

Maktaba hii inapatikana katika Jiji la Copenhagen, Aarhus na Denmark. Maktaba hii ni ya Kitaifa, Maktaba ya Chuo Kikuu, Kituo cha Kitaifa cha Huduma Zilizoshirikiwa kwa Maktaba za Umma.

I,maktaba ya Kifalme ya Denmark imehifadhi nyaraka zipatazo milioni 42,504,062 zinazoshikika. Na pia imehifadhi nyaraka za kielektroniki zipatazo 8,615,234.

Imeajiri wafanyakazi 800.




## 10. MAKTABA YA KITAIFA YA UCHINA (Kichina: 中国国家图书馆; NLC)

Hii ni maktaba ya kitaifa ya Jamhuri ya Watu wa Uchina, iliyoko Beijing, Uchina, na ni moja ya maktaba kubwa zaidi ulimwenguni. Ina zaidi ya nyaraka milioni 41 kufikia Desemba 2020. Inashikilia mkusanyiko mkubwa zaidi wa maandishi ya Kichina na hati za kihistoria ulimwenguni na ina ukubwa wa eneo la mita za mraba 280,000. Maktaba ya Taifa ni taasisi ya ustawi wa umma inayofadhiliwa na Wizara ya Utamaduni na Utalii.

**Msingi**

Mnamo mwaka wa 1906, gavana wa jimbo la Hunan Pang Hongshu alikalia kiti cha enzi na kutangaza kwamba alikuwa amekamilisha matayarisho ya kuunda maktaba ya mkoa huko Changsha. Mnamo 1908 na 1909, maofisa wakuu kutoka majimbo ya Fengtian, Shandong, Shanxi, Zhejiang na Yunnan waliwasilisha ombi kwa Mahakama ya Kifalme wakiomba ruhusa ya kuanzisha maktaba za umma katika eneo lao la mamlaka. Tarehe 2 Mei 1909, Wizara ya Elimu ya Qing (学部; 學部; Xuébù) ilitangaza mipango ya kufungua maktaba katika kila mkoa wa nchi.



## SHOW YOUR WORK

**Jina la kitabu-** Show your work
**Mwandishi-** Austin Kleon
**Msomaji–** Vrom
**Mkoa-** Dar

Mm nimejifunza kwanza ili watu wengine wakuone au wajue unachofanya sio lazima upate *audience* ya watu wakubwa wakusikilize ila ni kujaribu kujitangaza katika hz social media zetu kwa kuzingatia maudhui ya yale unayotaka watu wapokee na kujifunza zaidi kutoka Kwako.

Nimejifunza kuwa huhitaji mtu aku*push* ili uweze kufanya jambo, kinachohitajika ni kusimama, kuamua na kutenda bila kuogopa.

Jambo jingine ni kutokuruhusu roho ya uoga au kukata tamaa, ktk kila jambo lazima tuzingatie wapi tunataka kufika.

Nimejifunza pia katika kila kazi ambayo mtu anafanya lazima apate mirejesho mibaya na mizuri kwa hiyo tusiogope na tusichukulie *personal* maana kila mtu ana upeo tofauti na kuendelea na zile *comment* ambazo zinajenga kusonga mbele.


Nimejifunza kufanya kitu ambacho mimi ninakipenda ambacho nitafanya kwa nguvu zote bila ya kukata tamaa.

Nimejifunza kwamba kujua kitu hakumaanishi ndyo mwisho wa kujifunza. Kila siku tunatakiwa kujifunza vitu mbalimbali vipya ili kuboresha kile ambacho unacho au unakifanya.

Hili ni kubwa kuliko, nimejifunza ku*share* kile kitu ambacho nafanya ili watu wajifunze kutoka kwangu ambavyo itazidi kuonesha uwezo wa kile ninachofanya. Ndyo maana tunaona watu wenye kutoa sana kwa watu huwa wanakua kifikra, wanabarikiwa na kuzalisha zaidi kwasababu wameamua ku*share* na watu wengine.

Nimejifunza pia *work life balance*. Mwandishi anatusisitizia kuwa tuwe na muda wa kufanya kazi na muda wa kufanya mambo mengine kwa ajili ya ustawi wetu wa afya ya akili.

Kwa mfano kama unafanya biashara *then* uwe na muda wa ikizo iwe walau miezi 3 au sita au hata mwaka huku biashara ikiendelea bila kuathirika. Tunaita *having business continuity*. Wateja hawatateseka kupata huduma au bidhaaa.




**Je; wewe ni mmoja wa wanaopenda kusoma vitabu aina mbalimbali? Na hujui wapi au vipi utapata vitabu hivyo?**

**Anna Mbise Mobile Library ndiyo jibu lako. Jiunge sasa na mamia ya wasoma vitabu kwenye Anna Mbise Mobile Library.**

**Ukitaka kuwa mwanachama wa maktaba hii, tuma ujumbe "NIAZIME KITABU" kwenye Facebook Messenger.**

**Au piga simu namba: +255766069962**

Read & Write
With
Anna Mbise




**TANGAZA na NGURUMO YA MWANDISHI kwa bei nafuu na ya kirafiki.**
**Matangazo madogo ni Tsh 5000@ na Tangazo la kurasa nzima ni Tsh 10000@.**
**Wasiliana nasi kwa simu *(call & Whatsapp)* 0766974865 na Email: jamvilasimulizi@gmail.com**

**Jina la Shairi: Twacheni Siye Mafundi**

**Mtunzi: Salum Makamba "Mwanagenzi"**

Siye kutamba si kosa, washairi yetu jadi
Kwa tungo kunesanesa, wakale wetu uradi
Ambe hilo lamtesa, si malenga maridadi
Twacheni siye mafundi, fani tuipe hamasa

Fani tuipe hamasa, kwa tambo ziso idadi
Sithubutu kutugusa, bakini kutaradadi
Tumekwiva tena hasa, twanukia ka waridi
Twacheni siye mafundi, fani tuipe hamasa

Wakati tulio sasa, namba yetu ni wahedi
Aliyetupa furusa, si mwingine ni Wadudi
Shetani sije wanasa, mkatuumbia kedi
Twacheni siye mafundi, fani tuipe hamasa

Mje tuwape darasa, kutunga zilo jadidi
Ili mwache magarasa, kuyaumba kwa juhudi
Ama tena mtakosa, mje nguruma ka radi
Twacheni siye mafundi, fani tuipe hamasa

Tama tambo siyo kosa, bali yetu itikadi
Hata aletaye posa, ilipo yetu baladi
Siye yeye humuasa, kutamba pasi idadi
Twacheni siye mafundi, fani tuipe hamasa

***Salum Makamba "Mwanagenzi" ni mshindi wa Tuzo ya Mabati Safal Cornell mwaka 2022 katika utanzu wa ushairi.***

***Ni mshairi, mwigizaji, mwanahabari na ni daktari wa binadamu.***

***Salum Makamba ni hazina ya ushairi kwa vizazi vijavyo maana uandishi wake si wa karne hii.***

**Tanzania Tunalia**

Vilio masikitiko, Tanzania tunalia
Limekuja tikisiko, Bara Visiwani pia
Tumebaki na tanziko, fikra tukifikiria
Tanzania tunalia, Lowasa baba kwaheri

Wamasai wanalia, ndugu wamempoteza
Alowajali sawia, utu wake kuwekeza
Na taifa tunalia, chuma tumekipoteza
Tanzania tunalia, Lowasa baba kwaheri

Lowasa baba kwaheri, asante twakupatia
Tuliishi sote kwa heri, mengi ukatufanyia
Mema ya kutoka Monduli, bado tuna-kumbukia
Tanzania tunalia, Lowasa baba kwaheri

Pigo lisilo kifani, likatufikia pia
Babu aliye kufani, wosia katuachia
Tuwe hadithi kifani, wengine kuhadithia
Tanzania tunalia, baba Mwinyi umeenda

Baba Mwinyi umeenda, simanzi metuachia
Mengi kwetu umetenda, mwalimu rais pia
Sote si tulikupenda, manenoyo kucheshia
Tanzania tunalia, baba Mwinyi umeenda

Unguja wakulilia, na hata wa Pemba pia
Muda uliutumia, haki kuwapigania
Mema tutakuombea, nawe tuombee pia
Tanzania tunalia, baba Mwinyi umeenda

Pole Rais Samia, na Hussein Mwinyi pia
Ya Mungu yametimia, hatuna budi tulia
Zawadi litupatia, vema kumshukuria
Mwinyi Lowasa kwaheri, laleni pema peponi

***Shujaa Maneno—Bagamoyo Pwani***

**Unaweza kuchangia chochote ili kuwezesha jarida hili kuwa bora na kuwafikia wengi zaidi. Kama upo tayari, changia kiasi chochote kupitia MPESA LIPA NAMBA 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Na Mungu atakujazi.**


# Habari Picha




Mwandishi  Boniphace Ngumije katika picha ya pamoja na Naibu Waziri wa Sanaa na Michezo.



Mzee Richard Mabala katika moja na mbili na wapenzi wa vitabu vyake walipokutana kwenye mgahawa wa Swahili Food huko Kinondoni.






Eva Mrema katika picha ya pamoja na waasisi wa Swahili Food. Picha hii ilipigwa katika tukio la uzinuzi wa kitabu MWANAMKE MWENYE THAMANI NANI YANGU ukiofanyika Golden Tulip, 'Salaam.

**Ukilipata jarida hili, mtumie na mwezako.**

**"Tuambukizane furaha kwakuwa siyo ugonjwa"**
**by Luvanda Vitenge**

**'VITUKO VYA UHURU' - Harakati za kupigania Uhuru wa Tanganyika na vituko vyake. Ni kitabu kilichoandikwa na M.W. Kanyama Chiume—1973. Hii ni Kutoka Maktaba**

**Mwenyeji wao Ndugu Abdala Ali, alifungwa miezi sita. Chifu Mtoahanje wa Kiberege, alikataa kabisa kuingilia uamuzi wa chifu wake mdogo ili kuwaacha huru watu hao.**

Huko Mahenge, D.C. (aliyehusika baadaye na kesi ya Mwalimu Nyerere), alikataa kuwaona kwa muda wa siku saba na hatimaye alipokubali alikataa kabisa kuwapa ruhusa kufanya mikutano. D.C. huyo pia aliwatisha wananchi kuwaogofya wasiwe na uhusiano na wajumbe hao. Ilikuwa taabu kwa ndugu Lila na mwenzake kupata hata mahali pa kulala! Mganda mmoja, Ndugu Serujongi, akiwa karani bomani, kwa kuwaibia aliwapa nyumba mpya ya Idara ya Ujenzi kwa malazi kila siku baada ya kuhakikisha kwamba hakuna mtu aliyewaona wakiingia ama kutoka nyumbani humo! Ndugu Salumu Msafiri (aliyejiuzuolu kazi serikalini kutokana na kuchomwa na maneno makali ya Mwalimu aliporejea toka UNO) alijitolea kuwapa chakula.

Ilipokuwa dhahiri kwamba D.C. hasingewaruhusu kufanya mkutano wilayani, Ndugu Salumu Msafiri na wenzake wakaamua kufanya mkutano wa siri porini Ukwamu. Watu walipotoka tu kanisani, saa nane za mchana, kila mmoja alishika njia yake (ili asionekane), kuelekea sehemu hiyo. Tawi la siri la TANU likaundwa chini ya Ndugu Mohamed Mlolele akiwa mwenyekiti wa wilaya.

Mara baada ya wanachama kutawanyika, kila mmoja akiwa amepikwa vyema ki-TANU, kadi zilizofichwa na Nugu Mponji kwa mwalimu Ntanga, zilianza kuuzwa kwa siri. Mkutano huo wa siri uliamua pia kwamba, Ndugu Lila na mwenzake wangeenda Utengule kumwona Mtemi Towagale kuwaruhusu kufungua tawi la TANU malinyi.

Safari hiyo ilianza mara moja. Wakiwa njiani, Nduna wa Lupilo aliwaita mkutanoni watu wake na kuwakataza wasiwape chakula wala malazi. Huko Mtimbira walikutana na basi likiwa limewachukua vijana waliouomba ujumbe wao kuja Ulanga, wakipelekwa jela Mahenge kwa kifungo cha miezi sita eti, kutokana na hukumu ya chifu waliyekuwa wanamfuata, kwa kwenda Dar es salaam kuonana na Nyerere!

Ndugu Lila na mwenzake walikataliwa kabisa kufanya mkutano ama kufungua tawi la TANU huko. Akiona wanamkera kwa vile kila siku wao na wenyeji wao, Johari Binti Njaramoto, waalimwendeaa kumwomba ruhusa, akawashauri waende Utengule kuonana na baba yake kwa vile yeye hakuwa na uwezo waa kutoa kibali kama hicho!

Kama alivyohisi Binti Njaramoto pendekezo hilo lilikuwa mpango mbaya kwa ujumbe ule. Wajumbe ilikuwa lazima wavuke mto mkubwa wenye mamba ili kufika Utengule. Kwa hiyo licha ya kushauriwa kutokubebaa vitu vizito, Bwana Mpapai, mmoja wa wenyeji wao, aliwakabidhi pia vijana wawili wengine kufuatana nao pamoja na wale wawili ambao Karim, mwana wa Mtemi Towagale, aliwapa. Msafara ukiongozwa na Ruvu, kaka yake Karimu, ulidamka asubuhi na mapema, kuelekea Utengule.

"Tulipoingia tu katika mtumbwi kuvuka mto Rufiji (Mpanga)," alisema Ndugu Lila, "ikawa balaa kubwa. Wale vijana wa Karimu waliutingisha mtumbwi ukapinduka nasi tukajikuta majini—tumetoswa. Mwenye mtumbwi na vijana waliotumwa na Karimu kutuvusha wakatimkaa na kwenda zao huku wakipiga mayowe kwa furaha kwamba *Watu wa TANU wafile*—yaani watu wa TANU wamekufa. Wale vijana wawili waliotumwa kutisaidia walijitahidi kutuokoa kwa kuogelea na tukaponea chupuchupu kwa kushika magugu hadi ufukoni, lakini vitabu na makaratasi yetu, mablanketi na moja ya baiskeli mbili tulizoazima vilichukuliwa na maji."

"Tulipofika ufukoni tu," aliendelea, "tulikata mbuga ovyo na tukafika Utengule baada ya mwendo wa saa tano ama sita. Huko pia tukakuta sherehe kubwa sana na huku watu kwa mamia wanaimba *Watu wa TANU wafile.*

***Itaendelea toleo lijalo...***

# Sheria ya ndoa katika mgawanyo wa mali pindi ivunjikapo



***Ameandika Comred Mbwana Allyamtu***

Jana nimeulizwa swali kuhusu sheria ya ndoa.

Swali lenyewe...

Mimi na mke wangu tumeishi miaka kadhaa bila kujenga, naye ni *housewife (mama wa nyumbani)*, wakati mimi nafanya kazi.

Baadae nikaenda benki na kupewa mkopo, nikanunua kiwanja kwa jina langu na kujenga. Mkopo huo nikawa nau *service* (marejesho) toka kwenye mshahara wangu. Je,

1. Ikiwa tutaachana wakati muda wa kurejesha mkopo haujaisha, anayo haki ya mgawo katika nyumba hiyo?

Jibu langu...

Kwakuwa hiyo mali imepatikana mkiwa kwenye ndoa, basi mkitengana itaingia kwenye mgawanyo pasipo kujali ulikopa wewe au kiwanja kipo kwa jina lako. Bado mwenzi wako anahesabika anamchango kwenye upatikanaji wa hiyo nyumba (au mali ambazo zinaweza kuwa kabati, sufuria n.k). Linapokuja suala la kugawana mali wengi hudhani mtindo unaotumika ni ule wa nusu kwa nusu, (50 kwa 50).

Hakika huo si mtazamo wa Sheria ya Ndoa, 1971 Sura ya 29 iliyofanyiwa marekebisho, mwaka 2002 bali ni Mtazamo wa Mitaani. Msingi uliowekwa na Sheria tajwa hapo juu ni kiwango cha mchango wa Mwanandoa katika kupatikana kwa mali bishaniwa.

Katika suala hilo kiwango alichochangia mwanandoa katika kupatikana kwa mali ndicho kitakachokadiriwa kuwa ndicho anakachostahili kupata. Mfano; Kama ni nyumba ya vyumba sita (6) mmoja anaweza kupata chumba kimoja (1) na mwingine vyumba (5) kutegemea na mchango wa kila mmoja. Aidha, mchango siyo lazima iwe leta nilete au Shilingi kwa Shilingi bali hata kazi za nyumbani anazofanya Mama/Mke au Baba/Mume wa nyumbani ambaye hana kipato zenyewe nazo huhesabika kama mchango katika kupatikana kwa mali husika.

Katika kutenganisha mali za wanandoa, mali hizo huwekwa kwenye makundi makuu matatu:

**KUNDI LA KWANZA:**

Mali ambazo mmoja kati ya wanandoa alikuwa nayo kabla ya kuoana au alikuja nayo wakati anaingia kwenye ndoa. Mfano: Mwanamke au mwanaume ameolewa au kuoa akamkuta mwenzake tayari ana nyumba yake basi hiyo haitachukuliwa kuwa ni mali ya ndoa.

## ELIMU JAMII:

# Sheria ya ndoa katika mgawanyo wa mali pindi ivunjikapo

**KUNDI LA PILI:**

Mali ambazo zimepatikama wakati wawili hao wakiwa tayari, ndani ya ndoa. Mfano: Ndoa imefungwa wawili wakaanza kuishi pamoja kwa taratibu wakaanza kujenga nyumba na kuikamilisha. Vifungu vya 59 na 60 (b) vya Sheria ya Ndoa, vinahusika.

**KUNDI LA TATU:**

Mali ambazo zimepatikana kwenye ndoa lakini hazina uhusiano wa kindoa. Mfano: Mmoja wa wahusika kurithi au kuzawadiwa mali fulani. Kifungu cha 61cha Sheria ya Ndoa kinaelezea.

**KABLA NA BAADA YA NDOA:**

Mali iliyopatikana kabla ya ndoa na ikaendelea kuwapo kipindi cha ndoa inaendelea kuwa ya huyo mmliki, bila ushirika wa mwenza wake, kwa mujibu wa kifungu cha 58 cha Sheria ya Ndoa.

Kama ni nyumba mwanamke alikuwa nayo kabla ya kuolewa au ni mwanaume alikuwa anamiliki basi inaendelea kuwa ya kwake peke yake na haihusiki katika mgao pindi itakapohitajika kufanya hivyo.

Hata hivyo, Mali husika inaweza kuingizwa katika mgao ikiwa kuna mchango wowote wa kuiendeleza uliotolewa na mwenza (Mke au Mume) au kwa mhusika kuamua yeye mwenyewe bila kulazimishwa, mali ihusishwe kama mali ya familia au Mali ya Ndoa.

Zingatia...

Mkopo utaendelea kurejeshwa na aliyekopa hata ndoa ikivunjika maana yeye ndiye aliyeingia makubaliano na benki au taasisi hiyo ya kifedha.



*Ndimi,*

*Comred Mbwana Allyamtu CMCA*

*Sumbawanga Rukwa - Tanzania*

**Soma vitabu uupe afya ubongo wako**

**Soma vitabu ujifunze mengi mapya**

**Soma vitabu utembelee maeneo mbalimbali ya dunia kifasihi**

**Soma vitabu uburudike**

**“Aliyesoma kurasa moja ya kitabu kamwe hawezi kuwa sawa na asiyesoma kabisa”**

## Tangazo





www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi kila mwezi

jamvilasimulizi@gmail.com